
# MOYO WANGU WAMTUKUZA BWANA.

**LK.1.46-55**

Aron Reginald






2.Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amenitendea makuu ,*
Jina lake ni Takatifu.

3.Huruma yake kwa watu wanaomcha ,*
Hudumu kizazi hata kizazi.

4.Amefanya mambo makuu kwa mkono wake ,*
Amewatawanya wenye kiburi katika mawazo ya mioyo yao.

5.Amewashusha wenye vyeo kutoka viti vyao vya enzi ,*
Akawakweza wanyenyekevu.

6.Wenye njaa amewashibisha mema ,*
Matajiri amewaacha waende mikono mitupu.

7.Amempokea Israeli mtumishi wake ,*
Akiikumbuka huruma yake.

8.Kama alivyowaahidia wazee wetu ,*
Abrahamu na uzao wake hata milele.

9.Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu ,*
Kama mwanzo na sasa na siku zote /
Na milele amina.